



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO  
OFISI YA HAKIMILIKI TANZANIA



## TANGAZO

### **ONYO KWA WANAOKIUKA HAKIMILIKI KWA KUUZA KAZI ZA UBUNIFU KWENYE MITANDAO YA KIJAMII BILA RIDHAA ZA WAMILIKI HALALI WA KAZI HIZO**

Hivi karibuni kumekuwa na wimbi la watu mbalimbali kupitia mitandao ya kijamii kama vile *Telegram, WhatsApp, YouTube, Instagram* na kusambaza kazi za ubunifu kama vile tamthilia, filamu, picha, muziki, vitabu, machapisho n.k. kwa kuziua bila kuwa na kibali cha wamiliki halali wa kazi hizo, kufanya hivyo ni kosa kisheria kwani ni ukiukwaji wa Hakimiliki kinyume cha Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki Na. 7/1999 kama ilivyorekebishwa.

Hivyo, Ofisi ya Hakimiliki Tanzania (COSOTA) **INATOA ONYO KALI** kwa wasambazaji wa aina hiyo nchini na inawaagiza kuacha kusambaza kazi hizo za ubunifu zinazolindwa na Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki Na. 7 ya Mwaka 1999.

Kusambaza kazi hizo za ubunifu ni kosa kisheria kwa mujibu wa Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki na adhabu yake ikiwa utapelekwa Mahakamani ni faini isiyopungua kiasi cha shilingi milioni ishirini (20,000,000) au kifungo kisichopungua miaka 5 au vyote kwa pamoja. Pia adhabu ya kufifilisha makosa inayotolewa na COSOTA pasipo kufikishwa mahakamani ni faini hadi shilingi milioni ishirini (20,000,000).

Wananchi wenye taarifa za watu wanaojihusisha na shughuli za ukiukwaji wa Hakimiliki wanaombwa kutoa taarifa hizo kupitia namba ifuatayo **0738 015 013** au kutuma barua pepe ya [barua@cosota.go.tz](mailto:barua@cosota.go.tz) au kufika Ofisi ya COSOTA iliyopo Majengo ya Utumishi, Kivukoni. Donge nono litatolewa kwa yule atakayeweza kupatikana kwa anayekiuka hakimiliki ili kuzuia ukiukwaji huo.

Imetolewa na:  
**Kitengo cha Elimu na Uhusiano**  
**Ofisi ya Hakimiliki Tanzania (COSOTA)**  
**16/02/2024**



**Anitha Jonas**  
**AFISA ELIMU NA UHUSIANO**

